# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA RAIS
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**MKATABA**

**WA**

**KUUZA VIFAA VYA UJENZI WA JENGO LA EMD NA ICU HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA.**

Mkataba huu umefungwa leo tarehe ............. Mwezi .......... 2022

**KATI YA**

**Katibu Tawala, Mkoa wa Manyara, S.L.P. 310. BABATI, MANYARA (ambaye atajulikana kama Mnunuzi)** kwa upande mmoja

**NA**

**MANUU ENTERPRISES CO. LTD** wa S.L.P 236 Babati (**ambaye atajulikana kama Mzabuni**) kwa upande mwingine

**KWA KUWA Mnunuzi** yuko tayari kumpa **Mzabuni** kazi ya **kuuza vifaa vya ujenzi, wa** jengo la EMD na ICU Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara.

**Orodha ya vifaa vya ujenzi Pamoja na gharama zake ni kama ifuatavyo;**

| Item | Description of Goods | Quantity | Units | Agreed Rate |
|---|---|---|---|---|
| | **ICU GENERAL MATERIALS** | | | |
| 1 | Cement (42.5R/N) | 1 | bag | 17,000 |
| 2 | 16mm diameter (Min Tensile strength ≥460Mpa, BS4449.1997) | 1 | Pieces | 59,000 |
| 3 | 8mm diameter (Min Tensile strength ≥250Mpa, BS4449.1997) | 1 | Pieces | 15,000 |
| 4 | Binding wire (25kg roll) | 1 | Kg | 3,500 |
| 5 | Steel fabric reinforcement mesh ref. A142; weighing 4.5kg/m2; mesh size 200 x 200mm including tying wire and spacer. (2.4 x 27 Mtres per Roll) | 1 | Roll | 350,000 |
| 6 | 1.2 x 2.4m marine boards -18mm thick | 1 | piece | 70,000 |
| 7 | 2"x 3" x 3.6m softwood | 1 | piece | 5,000 |
| 8 | 1" x 8" x 3m treated softwood | 1 | Pieces | 16,000 |
| 9 | Concrete nails 2-4 Inch (According from Site Engineer) | 1 | Kg | 12,000 |
| 10 | 230mm wide gauge 500 laid over hardcore bed; Two layers DPM (2 x 200 mtres roll) | 1 | roll | 500,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11 | 230mm thick of hesian based bitumen felt DPC (1.2x 6mtrs roll) (1.2x 6 mtres roll) | 1 | roll | 120,000 |
| 12 | props (4" diameter) | 1 | pieces | 7,000 |
| 13 | Concrete nails 4 inches | 1 | Kg | 12,000 |
| 14 | 25mm Thick; compressible material i.e styropol or any approved material expansion joint set vertically between walling including sealing with any approved sealant material on both sides and cover up with Aluminum cap | 1 | $M^2$ | |
| 15 | 280x80mm weathered once, throated once reinforced with 12mm diamter rebars with link of 8mm diameter rebars at 250mm c/c. (Pre-cast Grade 20) | 1 | M | 15,000 |
| 16 | 150x50mm Rafters. 3 Meters long. (Structural timbers; softwood; pressure impreganated with Tanalith C; fixing bolts.) | 1 | | 9,500 |
| 17 | 150 x 50mm Bottom cord. 3 Meters long (Structural timbers; softwood; pressure impreganated with Tanalith C; fixing bolts.) | 1 | Pieces | 10,000 |
| 18 | 100x50mmthick; Wall plates. 3 Meters long (Structural timbers; softwood; pressure impreganated with Tanalith C; fixing bolts.) | 1 | Pieces | 7,000 |
| 19 | 50x50mm thick; Purlins.3 Meters long. (Structural timbers; softwood; pressure impreganated with Tanalith C; fixing bolts.) | 1 | Pieces | 3,700 |
| 20 | 100x50 Struts.3 Meters long. (Structural timbers; softwood; pressure impreganated with Tanalith C; fixing bolts.) | 1 | Pieces | 7,000 |
| 21 | Iron Nails 4" | 1 | Kg | 4,000 |
| 22 | Roof covering sloping not exceeding 45 degrees from horizontal.3.0 metres sheets.28-gauge pre-painted IT sheets: single length: supplied by ALAF or equal and approved. | 1 | sheets | 54,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 23 | Angle Ridge Cap, 225mm girth (1.8m long) | 1 | Pieces | 25,000 |
| 24 | Roof Nails 2" for IT Sheets | 1 | Kg | 9,000 |
| 25 | (a) Size 1800 x 2100mm high | 1 | No | 600,000 |
| 26 | (b) Size 1500 x 2100mm high Doors | 1 | No | 500,000 |
| 27 | (c) Size 1000 x 2100mm high Doors | 1 | No | 400,000 |
| 28 | (d) Size 900 x 2100mm high Doors | 1 | No | 350,000 |
| 29 | Prime quality Wrot Hardwood 145mm x 45mm Frame | 1 | m | 28,000 |
| 30 | 50 x 15mm Glazing beads | 1 | m | 10,000 |
| 31 | Panes over 0.5m$^2$ not exceeding 1.0 m$^2$ | 1 | M$^2$ | 7,000 |
| 32 | 100mm Long Brass butt hinges;stainless steel | 1 | Pairs | 8,000 |
| 33 | Three levers Mortice lockset complete - Union | 1 | Set | 80,000 |
| 34 | Silver Door Closer Code with Standard arm. | 1 | Set | 40,000 |
| 35 | Hydraulic Floor hinges for Double swing doors | 1 | No | 300,000 |
| 36 | 75mm Stst.Matt Symbols to be identified by users (Sample to be approved) | 1 | No | |
| 37 | Supply, assemble and fix the following purpose made heavy duty natural ALUMINIUM framed sliding windows; frames 100 x 2mm POWDER COATED finish; 8mm thick glass; all complete with all fittings; accessories and fasteners; all from an approved ALUMINIUM window specialist including MOSQUITO GAUZE and with profiles from an approved manufacturer fixing to blockwork and / or concrete work; silicon sealant and weatherstripping all to Architect Approval. (a)Overall size 1800 x 1800mm high; | 1 | No | 750,000 |
| 38 | (b) Overall size 900 X 1800 mm high; | 1 | No | 400,000 |
| 39 | (c) Overall size 1500 X 1800mm high; | 1 | No | 600,000 |
| 40 | (d) Overall size 1800 X 1200mm high; | 1 | No | 500,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 41 | (e) Grilles; comprising of 25 x 50 x 3mm RHS framing and 25 x 25 x 3mm RHS intermediate sections; in filled with 3 x 25mm flat bars; cut, bent and welded to pattern as specified by the Architect's drawings. | 1 | m2 | 70,000 |
| 42 | (a)500x500x8mm (7pcs per box) | 1 | Box | 45,000 |
| 43 | (b) Silver Grey Grout (Application 1kg to 7m²) | 1 | Box | 3,500 |
| 44 | (c) Spacer (100 Nos per package) | 1 | kg | 4,000 |
| 45 | (d) (100x600mm long; 25pc per box) | 1 | Box | 38,000 |
| 46 | (e) Silver Grey Grout (Application 1kg to 5m²) | 1 | Box | 4,000 |
| 47 | (f) 250 x 400 x 6mm Thick ceramic wall tiles; 15pc per box) | 1 | Box | 20,000 |
| 48 | Silver Grey Grout (Application 1kg to 5m²) | 1 | Box | 5,000 |
| 49 | Gypsum board 1.2m x 2.4 mm sheet (Ex Thailand | 1 | pcs | 25,000 |
| 50 | Fibre tape- | 1 | Pcs | 7,000 |
| 51 | Gypsum screws 3/4" ( | 1 | box | 8,000 |
| 52 | 50 x 50mm Timber Brande rings/Ceiling joist treated | 1 | Pieces | 4,000 |
| 53 | Wire nails | 1 | kg | 4,000 |
| 54 | Gypsum cornice 2.5 m long piece | 1 | pieces | 3,500 |
| | **Sub Total 1** | | | |
| | **EMD GENERAL MATERIALS** | | | |
| 55 | Cement (42.5R) | 1 | Bag | 17,500 |
| 56 | 16mm diameter ((Min Tensile strength ≥460Mpa, BS4449.1997)) | 1 | Pieces | 54,000 |
| 57 | 12mm diameter ((Min Tensile strength ≥460Mpa, BS4449.1997)) | 1 | Pieces | 34,000 |
| 58 | 8mm diameter (Min Tensile strength ≥250Mpa, BS4449.1997) | 1 | Pieces | 15,000 |
| 59 | Binding wire (25kg roll) | 1 | Kg | 3,500 |
| 60 | Steel fabric reinforcement mesh ref. A142; weighing 4.5kg/m2; mesh size 200 x 200mm including tying wire and spacer. (2.4 x 27 Mtres per Roll) | 1 | Roll | 350,000 |
| 61 | 1.2 x 2.4m marine boards -18mm thick | 1 | Pieces | 70,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 62 | 2"x 3" x 3.6m softwood | 1 | Pieces | 5,200 |
| 63 | Concrete nails 2-4 Inch (According from Site Engineer) | 1 | Kg | 12,000 |
| 64 | 230mm wide gauge 500 laid over hardcore bed; Two layers-DPM (2 x 200 mtres roll) | 1 | Roll | 500,000 |
| 66 | (1 x 20 mtres roll) DPC | 1 | Roll | 120,000 |
| 67 | props (4" diameter) | 1 | Pieces | 7,000 |
| 68 | Concrete nails 4 inches | 1 | Kg | 12,000 |
| 69 | 25mm Thick; compressible material i.e styropol or any approved material expansion joint set vertically between walling including sealing with any approved sealant material on both sides and cover up with Aluminum cap | 1 | $m^2$ | |
| 70 | 230mm thick Solid blocks: B.S 2028: 450 x 150 x 230mm | - | No | 1,900 |
| 71 | 280x80mm weathered once, throated once reinforced with 12mm diamter rebars with link of 8mm diameter rebars at 250mm c/c. (Pre-cast Grade 20) | 1 | m | 15,000 |
| 72 | 150x50mm 3.6 Meters long treated | 1 | Pieces | 10,000 |
| 73 | 100x50mmthick; 3.6 Meters long treated | 1 | Pieces | 7,000 |
| 74 | 50x50mm thick; Purlins.3 Meters long | 1 | Pieces | 3,700 |
| 75 | Iron Nails 4" | 1 | Kg | 4,000 |
| 76 | Fascial/Barge board;1" x 8" x 3m treated softwood | 1 | Pieces | 18,000 |
| 77 | 63 mm Diameter black pipes x 4mm thick | 1 | m | 25,000 |
| 78 | 35mm Diameter x 4mm thick struts | 1 | m | 18,000 |
| 79 | 200x50x2mm Zed purlins, including fixing angle iron cleats with bolts | 1 | m | 15,000 |
| 80 | 6mm Thick mild steel base plate size 300 x 300, holed twice for 16mm bolt, anchored to concrete work, painted (Bolt measuerd separatery) | 1 | No | 20,000 |
| 81 | 16mm. Diameter 250mm long mild steel anchor bolt with two nuts and washers treated with ant-rust solution casted to concrete. | 1 | No | 15,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 82 | 4mm thick mild steel angle plate 100x100mm, holed two times for 16mm bolts | 1 | No | 10,000 |
| 83 | 10mm thick mild steel angle plate 200x200mm, holed four times for 22mm bolts | 1 | No | 30,000 |
| 84 | 16 mm diameter mild steel bolt 150mm long and two nuts and washers | 1 | No | 13,000 |
| 85 | Suspended slab | 1 | $m^2$ | 15,000 |
| 86 | 3.0 metres sheets | 1 | Sheet | 54,000 |
| 87 | Angle Ridge Cap, 225mm girth (1.8m long) | 1 | Pieces | 25,000 |
| 88 | Roof Nails 2" for IT Sheets | 1 | Kg | 9,000 |
| 89 | Size 2780x2100mm high | 1 | No | 950,000 |
| 90 | Size 1540x2100mm high Doors | 1 | No | 530,000 |
| 91 | Size 1500x2100mm high Doors | 1 | No | 500,000 |
| 92 | Size 1200x2100mm high Doors | 1 | No | 450,000 |
| 93 | Size 900x2100mm high Doors | 1 | No | 350,000 |
| 94 | Size 800x2100mm high Doors | 1 | No | 300,000 |
| | Prime Quality Wrot Hardwood (Mkongo or Mninga) | | | |
| 95 | 145mmx45mm Frame | 1 | m | 28,000 |
| 96 | 50mmx15mm Glazing beads/ Mninga/mkongo | 1 | m | 4,000 |
| | 6mmthick toughed clear glass fixed with hardwood beads | | | |
| 97 | Panes over 0.5m2 not exceeding 1.0m2 | 1 | $m^2$ | 7,000 |
| 98 | 100mm Long Brass butt hinges;stainless steel | 1 | Pairs | 8,000 |
| 99 | Three levers Mortice lockset complete | 1 | Set | 80,000 |
| 100 | Silver Door Closer Code with Standard arm. | 1 | Set | 40,000 |
| 101 | Hydraulic Floor hinges for Double swing doors | 1 | No | 300,000 |
| 102 | 75mm Stst.Matt Symbols to be identified by users (Sample to be approved) | 1 | No | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 103 | Grilles; comprising of 25 x 50 x 3mm RHS framing and 25 x 25 x 3mm RHS intermediate sections; in filled with 3 x 25mm flat bars; cut, bent and welded to pattern as specified by the Architect's drawings. | 1 | $m^2$ | 70,000 |
| 104 | Overall size 3085 x 2000mm high; 8mm | 1 | No | 1,200,000 |
| 105 | Overall size 1800 X 1500 mm high; 8mm | 1 | No | 650,000 |
| 106 | Overall size 1500 X 1500mm high; 8mm | 1 | No | 550,000 |
| 107 | Overall size 1500 X 800mm high; | 1 | No | 400,000 |
| 108 | Overall size 1300 X 1500mm high; | 1 | No | 600,000 |
| 109 | Overall size 1200 X 1500mm high; | 1 | No | 500,000 |
| 110 | Overall size 900 X 1500mm high; | 1 | No | 450,000 |
| 111 | Overall size 1200 X 1200mm high; | 1 | No | 400,000 |
| 112 | Overall size 900 X 800mm high; | 1 | No | 350,000 |
| 113 | 500 x 500 x 8mm Thick porcelain tiles; laid to falls sloping not exceeding 15 degrees from horizontal including staircase,landing and lamps. | 1 | $m^2$ | - |
| 114 | (500x500mm; 7pcs per box) | 1 | Box | 45,000 |
| 115 | Silver Grey Grout (Application 1kg to 7m²) | 1 | kg | 3,500 |
| 116 | Spacer (100 Nos per package) | 1 | Box | 4,000 |
| 117 | 150mm Skirting | 1 | Box | |
| 118 | (100x600mm long; 25pc per box) | 1 | Box | 38,000 |
| 119 | (250x400mm; 15pc per box) | 1 | Box | 20,000 |
| 120 | Silver Grey Grout (Application 1kg to 5m²) | 1 | kg | 3,500 |
| 121 | a)1.2m x 2.4 mm sheet (Ex Thailand | 1 | Pcs | 25,000 |
| 122 | b) Fibre tape | 1 | Pcs | 7,000 |
| 123 | c) Gypsum screws | 1 | Box | 8,000 |
| 124 | 50 x 50mm Timber Branderings/Ceiling joist treated | 1 | Pieces | 4,000 |
| 125 | Wire nails | 1 | kg | 4,000 |
| 126 | Gypsum cornice2.5 m long piece | 1 | Pieces | 3,500 |

**NA KWA KUWA** Mzabuni yuko tayari na ana uwezo wa kufanya kazi hiyo:

**HIVYO BASI, WAHUSIKA WANAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

## 1: MAELEZO YA KAZI.

Kazi zinazotakiwa kufanyika ni kama ifuatavyo:

(i) Kuuza vifaa vya ujenzi kama tulivyokubaliana katika vikao vya kamati ya mazungumzo.

(ii) Kusafirisha vifaa hadi eneo la ujenzi, kuvishusha,na kuviweka eneo litakaloelekezwa na msimamizi wa kazi ndani la eneo la ujenzi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa.

(iii) Vifaa tajwa hapo juu vitakavyouzwa viwevimekidhi viwango vya ubora kama ulivyoelekezwa kwenye nukuu za bei.

(iv) Kutoa huduma ya kuleta vifaa hivyo kwa haraka pindi unapohitajika ili ujenzi usisimame.

## 2: MUDA WA KUKAMILISHA KAZI/MUDA WA MKATABA.

**Mzabuni** amekubaliana na **Mnunuzi** kuleta vifaa tajwa hapo juu kila vitakapohitajika kulingana na mahitaji/kiasi ambapo hata siku za mwisho wa wiki (weekend) atatakiwa kuleta vifaa vya ujenzi ikiwa atahitajika kufanya hivyo ili kazi isikwame na iwe ndani ya siku tatu tangu wakati wa kuagizwa vifaa husika.

Ieleweke wazi kuwa **Mzabuni** akishindwa kukamilisha kazi/kutoa huduma kwa muda waliokubaliana na **Mnunuzi**, atawajibika kumlipa Mwajiri fidia ya ucheleweshaji (liquidated damage) ya asilimia moja (1%) ya gharama ya mradi kwa kiasi cha kazi kilichobakia kwa siku kwa kila siku inayoongezeka baada ya kuvunja kipengele hiki cha Mkataba hadi atakapokamilisha kazi husika.

## 3. MALIPO KWA MZABUNI

Malipo kwa Mzabuni yatafanyika baada ya kuleta vifaa vikakaguliwa na Mnunuzi, vikakubaliwa na Mnunuzi, na Mnunuzi akatoa taarifa ya kuvikubali vifaa hivyo ndani ya siku mbili (2). Malipo ni kiasi cha fedha kile walichokubaliana (Mzabuni- **Manuu Enterprises co. Ltd** na Mnunuzi - **Katibu Tawala Mkoa wa Manyara**) kulingana na

masharti ya mkataba huu ambacho ni **Tshs. 568,890,500 (Milioni Mia Tano Sitini na Nane Laki Nane Tisini na Mia Tano tu.)**

Malipo yatafanyika kwa vifaa vitakavyoagizwa, vikaletwa na kupokelewa tu **(Malipo yatahesabiwa kwa kifaa kimojakimoja kilichoagizwa, kikaletwa na kupokelewa)**. Gharama hizo zote zinajumuisha upakiaji, usafiri, upakuaji, upachikaji na kodi. Ieleweke kuwa nunuzi hatakubali wala kuwajibika na ongezeko lolote la gharama kwa Mzabuni ambalo litasababishwa na makosa ya makadirio ya Mzabuni mwenyewe kwa sababu yoyote ile katika utekelezaji wa mkataba huu.

## 4. MAJUKUMU YA WAHUSIKA:

### 4.1 Majukumu ya Mzabuni

**Mzabuni atatakiwa:**

(a) Kuleta vifaa vinavyohitajika na Mnunuzi kwa wakati na muda waliokubaliana.

(b) Kutoa Huduma kwa viwango vilivyooneshwa na ubora unaotakiwa na Mnunuzi

(c) Kuzingatia suala la kuhifadhi na kutunza mazingira wakati wote wa kufanya/kutekeleza wa Huduma hiyo;

(d) Kuzingatia uangalifu, uadilifu na uaminifu wakati wa kutekeleza Mkataba huu. Itakapobainika kuna udanganyifu katika kutekeleza kazi hii kinyume na makubaliano yaliyomo kwenye Mkataba huu, Mzabuni atalazimika kurejesha gharama zote za Mkataba huu na kufikishwa katika vyombo vya Sheria kwa hatua za kisheria zaidi;

(e) Kusafisha na kuandaa eneo la kuweka vifaa tajwa hapo juu.

## 4.2 MAJUKUMU YA MWAJIRI.

**Mwajiri atatakiwa:**

(a) Kumuwezesha Mzabuni kuwa na mazingira mazuri katika utekelezaji wa Mkataba huu, ikiwa ni pamoja na kutembelea kwenye eneo la Utoaji wa Huduma na kukagua ubora wa huduma na kutoa ushauri au maelekezo pale inapohitajika kulingana na mahitaji ya Mwajiri.

(b) Kumlipa Mzabuni stahiki yake kama makubaliano yalivyo. Ieleweke kuwa Mnunuzi hatalipa malipo yote Kwa Mzabuni kabla ya kukamilisha kiasi cha kazi aliyopewa kulingana na Mkataba huu. Aidha, Mwaj hatalipa kiasi chochote cha malipo kwa Mzabuni kama Mzabuni atashindwa kukamilisha kazi kwa wakati kulingana na Mkataba badala yake Mzabuni atatakiwa kulipa fidia ya ucheleweshaji vifaa kwa Mwajiri.

(c) Kukagua huduma inayotolewa na Mzabuni atatoa ushirikiano unaofaa wakati Mwajiri atakapohitaji kufanya hivyo.

## 5. MATUKIO YASIYOTARAJIWA (FORCE MAJEURE)

5.1 Matukio yasiyotarajiwa (*FORCE MAJEURE)* yana maana ya matukio yaliyo nje ya uwezo wa wahusika na ambayo hawakuweza kuyaona wakati wa kusaini Mkataba huu, ambapo matokeo yake yatasababisha Mzabuni asiweze kutekeleza Mkataba huu. Matukio hayo ni kama vita, vita vya kikabila, moto, mafuriko, mgomo, magonjwa ya mlipuko na mengineyo.

5.2 Matukio haya yatakapotokea wahusika wa Mkataba huu wataahirisha utekelezaji wa Mkataba huu bila kuwajibika kwa hasara itakayotokana na tukio husika, kwa kipindi na eneo linalohusika na lililoathiriwa na tukio husika.

5.3 Wahusika wa Mkataba huu watapeana taarifa haraka iwezekenavyo kabla ya kusimamisha kazi/huduma. Kama taarifa ya awali imetolewa kwa njia isiyo ya maandishi, ndani ya masaa 24 taarifa iliyotolewa kwa njia isiyo ya maandishi itolewe kwa maandishi. Mawasiliano yote ya maandishi yatawasilishwa kwenye ofisi ya Mwajiri na siyo sehemu nyingine yoyote.

## 6. UWAJIBIKAJI WA WAHUSIKA.

6.1 Mzabuni atawajibika kwa hasara, uharibifu na gharama zinazotokana na uzembe wake mwenyewe, mawakala wake au wafanyakazi wake wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu.

6.2 Mwajiri hatawajibika kwa hasara au uharibifu wowote utakaotokana na uzembe wa Mzabuni mwenyewe au Mawakala wake au wafanyakazi wake wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu.

## 7. KUSULUHISHA MIGOGORO:

7.1 Wahusika wa Mkataba huu watatumia uwezo wao wenyewe kusuluhisha kwa amani migogoro na tofauti yoyote itakayojitokeza kati yao inayohusu utekelezaji wa Mkataba huu.

7.2 Endapo watashindwa kusuluhisha mgogoro au tofauti kati yao, mmoja wao atawasilisha mgogoro huo kwa msuluhishi kulingana na **Sheria ya Usuluhishi Na.15 Sura Na. 15 /2002.**

7.3 Hatua ya mwisho itakuwa ni kwenda Mahakamani endapo wahusika watashindwa kusuluhisha mgogoro wao.

## 8. SHERIA ITAKAYOTUMIKA:

Mkataba huu utatafsiriwa na kuongozwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania.

## 9. MAELEKEZO/MAWASILIANO:

Maelekezo yanayotolewa na Mnunuzi yatakuwa kwa maandishi. Kwa sababu nyingine yoyote ile maelekezo hayo yanaweza yakatolewa kwa njia ya mdomo, Mzabuni atafuata maelekezo hayo. Katika muda usiozidi saa 72 Mnunuzi atatakiwa kuthibitisha kwa maandishi maelekezo aliyoyatoa awali kwa njia ya mdomo.

## 10. KUHAMISHA MKATABA/KUTOA KAZI KWA MZABUNI MSAIDIZI:

**Mzabuni** hatatoa kazi au sehemu ya kazi kwa Mtu/Kampuni nyingine bila kibali cha maandishi kutoka kwa Mwajiri. Kibali kama hicho kinapotolewa hakimwondolei **Mzabuni** mamlaka au majukumu yake chini ya Mkataba na **Mzabuni** atawajibika kwa kushindwa au kuzembea kwa yeyote kati ya wazabuni wake wasaidizi.

## 11. VIFAA VINAVYOWEZA KUKATALIWA:

Vifaa visivyokidhi mahitaji, viwango na maelekezo ya Mnunuzi kama ilivyoelekezwa kwenye Mkataba vitakataliwa na Mnunuzi. Kwa maelekezo ya Mnunuzi, Mzabuni kwa gharama zake mwenyewe atarekebisha/atabadilisha kifaa kitakachokuwa kimekataliwa hadi kumridhisha Mnunuzi kikamilifu. Endapo

Mzabuni atashindwa kufanya marekebisho au mabadiliko ya kifaa kilichokataliwa kwa wakati, Mwajiri atahesabu hasara itakayosababishwa na uzembe huo na mzabuni atawajibika kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 4.1 hapo juu.

**12. MABADILIKO YA BEI:**

Kwa kuzingatia kuwa wakati wote wa utekelezaji wa Mkataba huu bei ya kifaa/vifaa inaweza kubadilika kwa kupanda au kushuka, **Mnunuzi** na **Mzabuni,** watakaa pamoja na kufanya makubaliano mapya kwa kuzingatia mabadiliko halisi ya bei ya kifaa/vifaa husika katika soko kwa wakati huo.

Mabadiliko hayo yatazingatia bei katika soko ambalo kwa wakati huo ndilo Mzabuni ananunua vifaa husika. Kipengele hiki hakimlazimishi Mnunuzi kukubali mabadiliko atakayopendekeza Mzabuni.

**13. KUVUNJA MKATABA:**

13.1 Kama **Mzabuni** atashindwa kuanza kufanya kazi/kutoa huduma katika muda uliopangwa au kuna sababu za kutosha kuamini kuwa hatakamilisha kuleta vifaa vyote katika muda uliopangwa au kuna cheleweshaji uliokiuka tarehe na muda wa kukamilisha kutoa huduma au anashindwa kufuata moja ya masharti au hafuati maelekezo ya Mnunuzi au anakuwa mufilisi, Mnunuzi atakuwa na haki ya kuvunja mkataba na kumwajiri **Mzabuni** mpya wa kufanya kazi hiyo.

13.2 Kama Mnunuzi atashindwa kumlipa **Mzabuni** katika muda wa siku 28 baada ya tarehe ya kuwasilisha madai halali yaliyoidhinishwa na Kamati ya ukaguzi na upokeaji wa vifaa husika, Mzabuni atakuwa na haki ya kuvunja Mkataba. Pamoja na sababu hizo, sababu zifuatazo zinaweza kupelekea kuvunjika kwa Mkataba huu:

i. Kuwasilisha bidhaa ambazo ni chini ya kiwango kilichokubaliwa;

ii. Kuvunja sharti lolote la Mkataba huu.

**14. MALIPO BAADA YA MKATABA KUVUNJIKA:**

Kama Mkataba umevunjika, **Mzabuni** atalipwa na Mwajiri fedha au maamuzi yatakayokuwa bado hayajalipiwa katika malipo atakayokuwa amelipwa **Mzabuni** kwa Huduma yote itakayokuwa imetolewa kwa Mwajiri kabla ya kuvunjika Mkataba kwa kima na bei kama ilivyotolewa kwenye Mkataba.

**15. TAMKO LA MZABUNI**

15.1 Mimi ...MANUU ENTERPRISES CO. LTD... ambaye ni ...MKURUGENZI... natamka wazi kwamba nimefanya utafiti wa kutosha kwa ajili ya Kufanya kazi/kutoa huduma hii ya kuuza vifaa vya ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa jingo la EMD na ICU Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara kwa gharama ya **Tshs. Tshs. 568,890,500 (Milioni Mia Tano Sitini na Nane Laki Nane Tisini na Mia Tano tu.)**

Gharama zote hizo zinajumuisha usafiri pamoja na kodi, na kwamba, nisipotekeleza mkataba huu ipasavyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yangu kwa mujibu wa Mkataba huu. Pia natamka wazi kwamba **MZABUNI MANUU ENTERPRISES CO. LTD** siyo mtumishi wa ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Manyara, na kwamba endapo itathibitika nimedanganya hatua za kisheria zichukuliwe **dhidi yangu.**

Kwa ruhusa na kwa niaba ya Mzabuni:-

Jina ...DAVID J. MALEWA...

Saini ...[signature]...

Tarehe ...7.1.2022...

MANUU ENTERPRISES Co. LTD
0784-396054
07 JAN 2022
TIN:140-750-056
BOX 238 ... MANYARA

**ILI KUTHIBITISHA MAKUBALIANO HAYA, Wahusika wamesaini Mkataba huu kwa siku na tarehe kama inavyoonekana hapa chini:-**

**KWA UPANDE WA MNUNUZI MKATABA HUU UMESAINIWA NA:**

**JINA:** KAROLINA MTHAPULA

**CHEO:** RAS

**SAHIHI:** [signature] KATIBU TAWALA MKOA WA MANYARA

**ANUANI:** S.L.P 310, BABATI

**TAREHE:** 07/01/2022

**SHAHIDI:**

**JINA:** NEEMA GASABILE

**CHEO:** MWANASHERIA

**SAHIHI:** [signature]

**ANUANI:** 310 BABATI

**TAREHE:** 07/01/2022

WAKILI WA SERIKALI
07 JAN 2022
OFISI YA MKUU WA MKOA MANYARA

**KWA UPANDE WA MZABUNI MKATABA HUU UMESAINIWA NA:**

**JINA:** MANUU ENTERPRISES CO. LTD

**SAHIHI:** [signature]

**ANWANI:** 236 BABATI

MANUU ENTERPRISES CO. LTD
Tel: 0784-396054
07 JAN 2022
TIN: ...

**TAREHE:** 07. 01. 2022

**SHAHIDI:**

**JINA:** LYDIA Y KASAIMI

**SAHIHI:** [signature]

**CHEO:** MZABUNI

**ANWAN:** 319 BABATI

**TAREHE:** 7/1/2022